

**KAMPENI**

EACC yafungua kongamano la vilabu vya uadilifu vyuo vikuu mjini Homa Bay

UK 3




**UCHUKUZI**

KENHA yaandama wasafirishaji laghai wa miwa kudhibiti ajali barabarani

UK 7

**MABADILIKO YA TABIA NCHI**

Wanasayansi waelezea hofu huku viwango vya juu vya maji vikiathiri korongo Ziwa Bogoria



Uk 11


www.mygov.go.ke

JANUARI 24, 2023

# MyGov.

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO No. 28/2022-2023


**Takwimu za Wiki**


**1.4b** Pesa KPA imetenga kufidia wale watakaopoteza ardhi zao kwa mradi wa eneo maalumu la kibiashara la Dongo Kundu

**60m** Gharama ya mashwa tatu ambazo zitagawiwa wavuvi katika kaunti za Pwani

**11,000** Kiwango cha maji ambacho bwawa la Masinga husambazia kaunti ya Machakos

**184** Idadi ya wasichana walioruhusiwa kurejea makwao baada ya kutoroka ukeketeaji Migori

# Serikali yatengea eneo Spesheli la Uchumi la Dongo Kundu Sh39b



Waziri Moses Kuria alisema kwamba maandalizi ya kuanzisha SEZ yanaendelea vyema, kuhakikisha kwamba kituo cha viwanda na ushughulikiaji wa mizigo katika mji ulio na bandari wa Mombasa kinajengwa

**NA MOHAMED HASSAN (KNA)**

Mipango ya kuanzisha Eneo Spesheli la Uchumi (SEZ) la Dongo Kundu kaunti ya Mombasa yanaendelea vyema baada ya serikali kutengea mradi huo Sh39 bilioni.

Waziri wa Biashara, Uwekezaji na Viwanda Moses Kuria alisema kwamba mradi huo utakaogharimu Sh39 bilioni utaharakisha na kutoa nafasi tofauti za ukuaji wa uchumi katika jiji hilo la pwani.

Akizungumza katika Makao Makuu ya Mamlaka ya Bandari ya Kenya mjini Mombasa, Kuria alisema maandalizi ya kuanzisha SEZ yanaendelea vyema, kuhakikisha kwamba kituo cha viwanda na ushughulikiaji wa mizigo katika mji ulio na bandari wa Mombasa kinajengwa.



Alisema kwamba lengo la Eneo Spesheli la Uchumi la Dongo Kundu ni kuimarisha ukosefu wa usawa wa kibiashara Kenya, uwekezaji, kuunda nafasi za kazi na usimamizi bora.

ENDELEA UK 2




Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dkt Tedros Adhanom Ghebreyesus, abeba bango lenye ujumbe wa kuangamiza kifua kikuu katika World Economic Forum katika Davos, Switzerland,wiki jana. Picha: Hisani

## WHO kuanzisha baraza la chanjo ya TB ulimwenguni

**NA JOSEPH OUMA NA ROLEX OMONDI (KNA)**

Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) litaanzisha Baraza la Ulimwengu la Chanjo ya Kifua Kikuu (TB) ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo unaouawa watu.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO Dkt Tedros Adhanom Ghebreyesus, alifichua kwamba mwaka wa 2021, karibu watu 10.6 milioni waliugua Kifua Kikuu na watu 1.6 milioni walikufa kutokana na ugonjwa huo kote ulimwenguni.

Dkt Ghebreyesus alieleza matumaini yake kwamba Baraza la Kuharakisha Chanjo ya Kifua Kikuu, itafaulu kuzuia athari hasi za janga la Covid-19 kwa ugonjwa huo.

“Hakuna chanjo mpya ya TB imewahi kutolewa kwa miaka 100. Uwezekano wa kuwa na chanjo bora za TB umeongezeka majuzi kukiwa na chanjo 16 zinazoandaliwa na kuthibitisha thamani ya chanjo,” alieleza.

Mkurugenzi Mkuu huyo alifichua hayo katika Mkutano wa Uchumi Ulimwenguni uliofanyika Davos, Uswizi, wakati wa kikao kupitia video na washiriki.

ENDELEA UK 2

“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




# Serikali yatengea eneo Spesheli la Uchumi la Dongo Kundu Sh39b

ENDELEA KUTOKA UK 1

SEZ ni maeneo yaliyoteuliwa kijiografia ambayo serikali huwa zinatumia kuinua shughuli za viwanda kupitia usaidizi wa miundomsingi na vichocheo vya kifedha na usimamizi.

Huwa yako na majina mengi, ikiwemo maeneo huru ya biashara na maeneo ya viwanda.

“Kuna haja ya serikali kuchukua hatua makusudi kuweka muundomsingi wa kutegemewa ili kuwezesha wawekezaji kufanya mipango ya muda mrefu ya uwekezaji,” alisema.

Akiandamana na Gavana wa Mombasa Abdulswamad Sharif Nassir, Makatibu wa Wizara Abubakar Hassan Abubakar ( Idara ya Serikali ya Uwekezaji) na Alex Wachira (Idara ya Serikali ya Kawi), Kuria alisema SEZ itajengwa katika ardhi ya ekari 3000.

Alisema kwamba mradi huo, ambao utaleta mabadiliko ya ukuaji katika eneo hilo, utakuwa na bandari huru,

> “Tutatangaza tenda ya ustawi wa ardhi kuvutia uwekezaji” –Kuria


Waziri wa Biashara, Uwekezaji na Viwanda, Moses Kuria akiwa na Gavana wa Mombasa, Abdulswamad Nassir alipotembelea bandari ya Mombasa.

eneo huru la biashara, eneo la viwanda, eneo la usafirishaji na eneo la kutumiwa na umma likiwa na barabara la kilomita 12

Waziri alisema kwamba watatoa tangazo kuvutia uwekezaji katika sekta muhimu za uchumi kama vile viwanda vya kutengeneza bidhaa za kilimo, mafuta na gesi, kemikali za viwandani, kawi salam, uchumi wa baharini na kuondo chumvi katika maji na utoaji wa huduma.

“Kwa sasa tunajiandaa kutoa tenda ya ustawishaji wa ardhi katika vyombo vya habari vya humu nchini na vya kimataifa ili kuvutia uwekezaji. Ni matumaini yetu kuwa, tenda zitatolewa ndani ya wiki moja au mbili na kazi itaanza Machi 31 2023,” alisema kwenye mkutano na wanahabari.

“Eneo Spesheli la Uchumi la Dongo Kundu ni mojawapo ya miradi ya Ruwaza ya 2030 katika eneo hili,” alisema.

Waziri aliongeza kuwa eneo hilo spesheli la uchumi linatarajiwa kuanza kazi kutoka Julai 2023, akisema kwamba muundomsingi ni nguzo ya maendeleo ya uchumi jamii na mradi huu mkubwa unaojenga unaonyesha hivyo.

Alifichua kuwa KPA imetenga Sh1.4 bilioni kulipa fidia watu watakaohama makwao kutoa nafasi kwa mradi huo mkubwa.

# WHO kuanzisha baraza la chanjo ya TB ulimwenguni

ENDELEA KUTOKA UK 1

Alisema kwamba kwa nchi kuangamiza TB kufikia mwaka wa 2030, Baraza litawezesha utoaji wa leseni na matumizi bora ya chanjo za kifua kikuu.

Kwa njia hii, Baraza litaharakisha ushirikiano kati ya wafadhili, mashirika ya kimataifa, serikali na watumiaji kutambua na kukiuka visiki vya utengenezaji wa chanjo ya TB.

“Mojawapo wa mafunzo muhimu tuliyojifunza katika kukabiliana na janga la COVID-19 ni kwamba, kubuni mbinu za afya kunaweza kufanyika haraka iwapo kutapatiwa kipaumbele kisiasa na kufadhiliwa ipaswavyo,” alisema Dkt Ghebreyesus.

Alisema kwamba ingawa TB na Covid-19 zinasababisha changamoto tofauti, vigezo vinavyoharakisha sayansi, utafiti na ubunifu kwa wakati mmoja, na kwa hivyo vinafaa kuwa dharura, kupatiwa kipaumbele katika ufadhili wa umma; usaidizi kutoka mashirika wafadhili; majadiliano na sekta ya kibinafsi na jamii.

WHO inaamini kwamba nyanja ya TB itanufaika pakubwa kutoka kwa ushirikishi wa hali ya juu wa Baraza hili mpya na nchi wanachama.

Shirika hilo la ulimwengu linahofia kuwa gonjwa hilo halionyeshi dalili za kupungua licha ya nchi kuahidi kuangamiza TB kufikia 2030 inavyotarajiwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mkakati wa WHO wa kuangamzia TB na makubaliano ya kisiasa yam waka mwa 2018 kuhusu vita dhidi ya gonjwa hilo.

Kwa wakati huu, chanjo ya Bacillus Calmette – Guerin (BCG) inabaki kuwa chanjo ya pekee iliyopatiwa leseni na inazuia aina hatari za ugonjwa huo katika watoto wanaozaliwa wale wachanga, taarifa iliyotolewa kwa wanahabari ilisema. Hata hivyo, stakabadhi hiyo inasema kwamba BCG haikingi matineja na watu wazima inavyopaswa ambao ni asilimi 90 ya wanaosambaza TB ulimwenguni.

National Irrigation Authority

## TENDA WAZI YA KIMATAIFA

National Irrigation Authority inaalika maombi yaliyofungwa kwa tenda zifuatazo:

| S. NO | NAMBARI YA TENDA | JINA LA TENDA | TAREHE YA MWISHO | KUNDI LENGWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | NIA/T/144/2022-2023 | Ukarabati na Kuboresha Kituo cha Kusambaza Maji katika Ahero Irrigation Scheme, kaunti ya Kisumu | Februari 16, 2023 saa 6.00 mchana saa za Afrika Mashariki | Taasisi zilizosajiliwa Hungary |

Stakabadhi ya tenda ambayo inajumuisha mahitaji ya awali ya lazima, vigezo vya kifedha vya kufanya utathmini zinaweza kukaguliwa na kupatikana na waliohitimu kutuma maombi ***bila malipo*** kutoka kwa mtandao wa Mamlaka: http://www.irrigation.go.ke/tenders au lango la serikali kuu la uagizaji bidhaa kwa njia ya kieletroniki http://www.supplier.treasury.go.ke kuanzia **Januari 24, 2023**. Wanaonuia kutuma maombi **LAZIMA** wawasilishe majina na maelezo yao kwa haraka kwa: purchasing@irrrigation.go.ke au enquiries@irrigation.go.ke kwa mawasiliano kuhusu ufafanuzi au maelezo ya ziada wakati wa mchakato wa kupeana tenda..

**Anwani**
**Chief Executive Officer/CEO**
**National Irrigation Authority (NIA)**
**Irrigation House,**
**Lenana Road, Hurlingham, Nairobi, Kenya**
**Tel: +254-20-2711380/468**
**Fax: +254-20-2722821/2711347**
**E-mail: ceo@irrigation.go.ke; purchasing@irrigation.go.ke**

**AFISA MKUU MTENDAJI/CEO**
**NATIONAL IRRIGATION AUTHORITY**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

HUDUMA KWA TAIFA — NATIONAL YOUTH SERVICE

## HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA

## TANGAZO LA ZABUNI

**NAMBA. NYS/PROC/027/2022-2023**

**UWEKAJI ALAMA NA UFUATILIAJI MALI ZISIZOHAMISHIKA NA ZINAZOHAMISHIKA KATIKA HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA**

**HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA (NYS)** inakaribisha zabuni funge kutoka kwa Kampuni zinazostahiki kwa Mashirika ya Ununuzi ya Serikali (AGPO) katika Huduma ya Kitaifa kwa Vijana kwa utoaji wa huduma za Uwekaji Alama na Ufuatiliaji wa mali zisizohamishika zinazohamishika katika Huduma ya Kitaifa ya Vijana (Zabuni ya Wazi).

Seti kamili ya hati za zabuni inaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti za Huduma: www.nys.go.ke au kutoka kwa tovuti ya Hazina ya Kitaifa: http//supplier.treasury.go.ke ***bila malipo*** au Ksh.1,000 zitatozwa kwa kupata hati kutoka makao makuu ya NYS inayolipwa kwa pesa taslimu kwa NYS au hundi ya benki.

Wazabuni lazima wajaze fomu maalum ya kupata Zabuni.

Bei zilizonukuliwa zinapaswa kujumlisha ushuru wote, lazima ziwe katika Shilingi za Kenya na zitaendelea kuwa halali kwa siku (120) kuanzia tarehe ya kufungwa ya zabuni.

Hati zilizokamilishwa za zabuni zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha iliyotiwa muhuri wazi iliyotiwa alama ya nambari ya zabuni na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni katika Makao Makuu ya NYS, Ruaraka, ghorofa ya kwanza ili kupokelewa mnamo au kabla ya tarehe **8 Februari, 2023 saa 10.00 asubuhi** zitumwe kwa:

**MKURUGENZI MKUU/CEO**
**MAKAO MAKUU YA HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA**
**P. O. Box 30397-00100**
**NAIROBI.**

Zabuni zitafunguliwa mara moja baada ya hapo saa **10.00 asubuhi** mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika Makao Makuu ya NYS, Ruaraka.

**MKUU WA URATIBU WA HUDUMA ZA USAMBAZAJI**
**KWA: MKURUGENZI MKUU/CEO**

KENYA VISION 2030






# EACC yafungua kongamano ya vilabu vya uadilifu vyuo vikuu Homa Bay

BY BRIAN ODHIAMBO AND SITNA OMAR (KNA)

Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC) imefungua kongamano la kwanza la uadilifu katika vyuo vikuu eneo la Nyanza linalolenga kukuza tabia na hulka za vijana.

Kongamano hilo la siku mbili lenye mada " kuunda maadili kupitia vilabu vya uadilifu vyuoni" lilifanyika katika Chuo Kikuu cha Tom Mboya mjini Homa Bay.

Vilabu vya uadilifu katika shule na taasisi za masomo ya juu vilianzishwa na Wizara ya Elimu, kwa ushirikiano na EACC kusaidia kuzuia changamoto za ufisadi katika umri mdogo.

Hafla hiyo ilileta pamoja viongozi wa wanafunzi kutoka vyuo vikuu katika eneo la Nyanza, vikiwemo Tom Mboya, Maseno, Kisii, Rongo, Great Lakes Kisumu, Jaramogi Oginga Odinga na Uzima.



Mkurugenzi wa EACC, Vincent Okongo, akihutubia wadau waliohudhuria kongamano la vilabu vilabu vya maadili vyuo vikuu vya Nyanza katika Tom Mboya University. (PICHA: Brian Odhiambo)

Akazungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa kongamano hilo, Mkurugenzi wa Huduma za Kinga katika EACC, Vincent Okongo alisema kwamba kongamano hilo linawapatia jukwaa la kubadilishana mbinu bora katika vilabu hivyo vya uadilifu katika vyuo vikuu kadhaa katika eneo pana la Nyanza.

Kulingana na utafiti uliofanywa na EACC na kutolewa Desemba mwaka jana, changamoto ya ufisadi katika vyuo vikuu inashuhudiwa hasa na vijana.

> Nina furaha matokeo ya juhudi za Tume yameonekana,- Okong'o

"Sekta imejawa na ufisadi na wengi wao wanatoka vyuo vikuu, hali inayotufanya kuleta pamoja viongozi wa vyuo vikuu kwa mafunzo," alisema Okong'o.

Mkurugenzi alisema kwamba mpango huo ni sera ya muda mrefu ya Tume, inayolenga kuwa na jamii inayoongozwa na maadili.

"Niko na furaha athari za juhudi za tume zimeanza kuonekana, hasa kupungua kwa migomo katika taasisi za masomo," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza kuwa vijana wanaweza kudumisha maadili kwa kuwa watetezi wake katika jamii, wakiinua maadili mema na pia kwa kushiriki katika uongozi.

Kamishna wa kaunti ya Homa Bay, Moses Lilan, alisema kwamba kupiga vita ufisadi ni haki na jukumu la kila mtu katika jamii iwapo uovu huo utakabiliwa.

Lilan alisema kwamba ufisadi unasababisha ukiukaji wa haki za binadamu, unatoshia usalama, unazidisha uhalifu wa kupangwa, unaharibu uchumi na kuvunja nafasi za maendeleo na hivyo basi kunasa watu katika ulimbo wa ukosefu wa usawa na umasikini.

"Uadilifu hauwezi kununuliwa. Ni lazima utie bidii ili uweze kuupata uwe ndani yako," alisema Lilan.

# Kaunti ya Nakuru yapiga jeki sekta ya afya kwa kuwekeza zaidi katika uuguzi

NA ESTHER MWANGI (KNA)

Serikali ya kaunti ya Nakuru imetenga pesa zaidi kuwezesha wafanyakazi wake wauguzi na wakunga ili kuafikia upanuzi wa haraka na kwa gharama nafuu wa Afya bora Kwa Wote (UHC).

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Afya na Mipango wa kaunti hiyo Dkt Joy Mugambi alisema, wauguzi hutekeleza jukumu muhimu katika huduma za afya na ni muhimu katika kusimamia changamoto ibuka za afya enzi za kisasa.

Akizungumza katika mahafala ya nane ya chuo cha matibabu cha Nakuru West Medical College cha kanisa ya Presbyterian Church of East Africa (PCEA) Dkt Mugambi alisema kwamba wauguzi wako katika nafasi bora ya kuinua afya na kinga dhidi ya magonjwa zaidi ya kushirikisha na kusaidia makundi ya wahudumu wa afya ya msingi katika viwango vyote.

Alisema kwamba kuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa upanuzi nafuu wa UHC unategemea pakubwa mafunzo na kuwezesha wafanyakazi walipo, wakiwemo wauguzi na wakunga, kufanya kazi vyema zaidi.



Dkt Joy Mugambi

Mkurugenzi huyo alisema kwamba kutakuwa na athari chanya kuhusu jinsi UHC inaweza kuafikiwa haraka iwapo wauguzi na wakunga watawezeshwa kufanya kazi kikamilifu walivyofunzwa au kuchukua nyadhifa mpya katika kazi spesheli au zilizopanuliwa.

Alisema kwamba wakati zaidi kwa wakati huu wanatafuta huduma za afya katika hospitali za umma ikilinganishwa na zile za kibinafsi, alihusisha hatua hii na uamuzi wa serikali ya kaunti kuajiri wahudumu zaidi wa afya waliohitimu na kuzidisha shughuli za uhamasishaji wa afya kote katika kaunti hiyo.

Dkt Mugambi alitoa changamoto wa wauguzi wanaoanza kutafuta kazi kutumia ujuzi wao kuzuia vifo vya watoto na akina mama na maradhi ibuka kama Covid-19 ili kuinua utekelezaji wa UHC.

"Wauguzi wanaingia kutafuta kazi wakati mchango wao unahitajika kupunguza mianya inayoendelea kuongezeka ya wafanyakazi na hivyo basi wanapaswa kuzingatia kiapo chao cha kazi cha Florence Nightingale Hippocratic Oath kwa Wauguzi," alishauri mkurugenzi huyo.

Pia alishauri waliohitimu kupanua mawambo yao na kulenga nafasi nyingi zilizoko katika sekta ya afya ndani na nje ya Mipaka ya Kaunti hiyo na kujaza pengo la wafanyakazi katika sekta ya afya.

Dkt Mugambi alisema kwamba kuhitimu kwa wauguzi hao 17, ambao walituzwa diploma, kutapiga jeki juhudi za kaunti hiyo za kutoka huduma bora na zilizoimarishwa za afya.

Mwalimu Mkuu wa taasisi hiyo Bw Cyprian Madungu alisema kwamba kwa miaka 12 iliyopita, wauguzi 200 wamehitimu kutoka chuo hicho cha matibabu na akaongeza kuwa kinaanzisha mipango mipya ya mafunzo kukidhi mahitaji katika soko ikiwemo Rekodi na Habari za afya miongoni mwa kozi zingine.

MASINDE MULIRO UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

*University of Choice*

Tel, 0572505222/3 or 0733120020/2 or 0702597360, P.O. BOX 190 – 50100 Kakamega, Kenya
Email: info@mmust.ac.ke; procurementofficer@mmust.ac.ke , Website: www.mmust.ac.ke

NOTISI YA TENDA

Masinde Muliro University of Science and Technology inaalika wote waliohitimu kutuma maombi ya kushiriki tenda zifuatazo;

| NO | NAMBARI | JINA LA HUDUMA | DHAMANA | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MMUST/009/SPD/2022-2023 | Kununua, Kuleta, Kuweka na Kuzindua Jenereta | 100,000 | Wazi |

Mashirika yaliyohitimu yanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa afisi za ununuzi saa za kawaida za kazi. Stakabadhi za tenda zinaweza kupatikana na kupakuliwa BILA MALIPO kwenye tovuti ya Chuo: www.mmust.ac.ke au PPIP Portal: supplier.treasury.go.ke

Stakabadhi zilizojazwa na kufungwa kwenye bahasha iliyofunikwa na kuandishwa jina la Tenda na Nambari zinapasa kutumwa kwa;

Vice Chancellor
Masinde Muliro University of Science and Technology- MMUST
P. O. Box 190-50100
Kakamega

AU, kuwekwa ndani ya **Sanduku la Tenda** lililoko katika kiingilio cha Jengo la Afisi (ABA) Building katika Masinde Muliro University of Science & Technology (MMUST) Main Campus kwenye barabara ya Kakamega – Webuye Road, Kakamega na wala **si** mahali pengine ili kufika chuoni kabla ya saa **4.00** asubuhi mnamo **Ijumaa Februari, 10, 2023**. Ufunguzi wa stakabadhi za tenda utafanyika baada ya hapo mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wataamua kuhudhuria.

**Vice Chancellor**
**Masinde Muliro University of Science & Technology**

KENYA VISION 2030

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA MADINI, RASILMALI NA MASUALA YA BAHARI

### *IDARA YA MADINI*

## MWALIKO WA ZABUNI

| | |
|---|---|
| JINA NA MAELEZO YA ZABUNI: | ZABUNI YA NAFASI ZA KURUHUSU/KUKODISHA VIBANDA VYA WAUZAJI VITO, KITUO CHA BENKI NA MIKAHAWA KATIKA KITUO CHA VITO NA KUONGEZA THAMANI CHA VOI, VOI, KAUNTI YA TAITA TAVETA |
| Namba ya Tenda. | NAMBA YA TENDA. MOMB&MA/SDM/VA/OT/01/2022-2023 |

1. Wizara ya Madini, Raslimani na Masuala ya Bahari, Idara ya Serikali ya Madini inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wazabuni wanaostahiki kwa ajili ya kukodisha/kukodisha vibanda vya wafanyabiashara wa vito, benki na migahawa katika kituo cha vito na kuongeza thamani cha Voi, huko Voi, Kaunti ya Taita Taveta kwa kipindi cha miaka Mitatu (3 ) na uwezekano wa kuongezwa kwa miaka mitatu (3) zaidi.

2. Seti kamili ya hati ya zabuni inaweza kupatikana bila malipo na wazabuni wanaovutiwa kwa njia ya kielektroniki kutoka kwa tovuti **www.mibema.go.ke** au **tenders.go.ke.**

3. Hati za zabuni zilizokamilishwa zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha zilizofungwa zilizoandikwa: ***"Zabuni ya nafasi ya kukodisha/kukodisha kwa vibanda vya wauzaji vito, benki na mikahawa katika kituo cha vito na kuongeza thamani cha Voi, huko Voi, Kaunti ya Taita Taveta*** na LAZIMA iwasilishwe kwa anwani iliyoonyeshwa hapa chini mnamo au kabla ya tarehe **3 Februari 2023** saa **11.00 asubuhi EAT** au iwekwe kwenye kisanduku cha zabuni kilicho kwenye jengo la kazi za umma orofa ya 2.

4. Wazabuni wanashauriwa kuwasiliana na afisa madini wa kanda katika Kituo cha Vito na Kuongeza Thamani cha Voi kwa ajili ya kutembelea eneo la zabuni wakati wa siku za kazi.

**KATIBU WA WIZARA**
**IDARA YA MADINI**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

## NOTISI YA UMMA

## KUSIMAMISHWA KWA USAJILI WA WATAALAMU WA KUKAGUA MAZINGIRA

Mamlaka (tangu 2004) imesajili zaidi ya wataalamu 12,000 wa kukagua mazingira kuendesha Utathmini wa Athari kwa Mazingira (EIA) na kukagua kwa lengo la kuimarisha hali ya mazingira.

Ukaguzi wa sajili ya leseni za utendakazi za kila mwaka za wataalamu umeonyesha kuwa, ni chini ya asilimia 50 ya wataalamu waliosajiliwa ambao wanatekeleza majukumu yao.

Hii imetulazimu kusitisha Usajili wa wataalamu wapya kuwezesha Ukaguzi wa sajili hiyo na kulainisha utaratibu wa usajili kuanzia Januari 1, 2023 hadi Julai 31, 2023.

Katika kipindi hiki, utoaji wa leseni za kila mwaka za utendakazi kwa wataalamu waliosajiliwa utaendelea.

**MKURUGENZI MKUU**
**DISEMBA 21, 2022**

KENYA VISION 2030 :NemaKenya www.nema.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA UWEKEZAJI, BIASHARA NA VIWANDA

### *Idara ya Viwanda*

## NOTISI YA ZABUNI

## TANGAZO LA ZABUNI KWA HUDUMA ZA USALAMA NA WALINZI KWA IDARA YA SERIKALI YA VIWANDA KWA MWAKA WA KIFEDHA 2022-2023

Serikali ya Kenya kupitia Idara ya Viwanda inawaalika wazabuni wanaostahiki kwa zabuni ya **Huduma za Usalama na Walinzi** kama ilivyoonyeshwa hapa chini

| S/No. | Namba ya Zabuni | MAELEZO YA ZABUNI | DHAMANA | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MoITED/SDI/1/2022-2023 | HUDUMA ZA USALAMA NA WALINZI | KSHS. 100,000 | 8 FEBRUARI, 2023 |

Waombaji wanaovutiwa wanaweza kupata seti kamili ya hati za zabuni na maelezo ya kina kutoka kwa tovuti ya wizara ***www.industrialization.go.ke*** bila malipo yoyote au kutoka Ofisi ya Meneja wa Mfumo wa Usambazaji, **Idara ya Viwanda** katika **Jengo la NSSF Block A, Eneo la Mashariki, Orofa ya 16** wakati wa saa za kawaida za kazi baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa ya Kshs. 1,000 kwa kila seti ya hati ya zabuni kwa pesa taslimu au hundi ya benki inayolipwa kwa Katibu, Idara ya Serikali ya Viwanda. Wazabuni wanaopakua hati ya Zabuni wanashauriwa kujiandikisha katika ofisi ya Msimamizi Mkuu wa Mfumo wa Usambazaji kabla ya tarehe ya kufunga.

Nyaraka za zabuni zilizokamilishwa katika bahasha zilizofungwa na zilizowekwa jina la zabuni na nambari ya zabuni lazima zitumwe kwa;

***Katibu wa Wizara,***
***Idara ya Serikali ya Viwanda,***
***P.O. Box 30547-00100,***
***NAIROBI.***

na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni kwenye Orofa ya 16, Jengo la NSSF, Kitalu A, Upande wa Mashariki ili kufikia **Jumatano tarehe 8 Februari 2023** au kabla, saa**10.00 asubuhi.**

Bei zilizonukuliwa lazima zijumuishe VAT na kodi zote za Serikali na lazima zisalie halali kwa muda usiopungua siku Mia Moja na Kumi na Tisa (119) kuanzia tarehe ya kufunga.

Lazima wazabuni wawasilishe Dhamana ya Zabuni kwa kiasi kilichoonyeshwa hapo juu katika mfumo wa dhamana ya benki kutoka kwa benki ya biashara inayotambulika au Kampuni ya Bima iliyoidhinishwa na PPRA, halali kwa muda usiopungua siku Mia Moja na Hamsini (150) kuanzia tarehe ya ufunguzi wa zabuni.

Ufunguzi wa zabuni utafanyika katika Chumba cha mikutano kilichopo kwenye Orofa ya 23, Jengo la NSSF mara baada ya tarehe na wakati uliotajwa hapo juu mbele ya wazabuni au wawakilishi watakaoamua kuhudhuria.

**Katibu wa Wizara**
**Idara ya Viwanda**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

RBA
Retirement Benefits Authority

## NAFASI ZA KAZI

Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu (RBA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya 1997 kama shirika lenye mamlaka ya kisheria ya: kudhibiti na kusimamia uanzishaji na usimamizi wa miradi ya mafao ya kustaafu; kulinda maslahi ya wanachama na wafadhili wa sekta ya mafao ya kustaafu; kukuza maendeleo ya sekta ya mafao ya kustaafu; na kumshauri Katibu wa Baraza la Mawaziri kuhusu sera ya kitaifa ya kufuatwa kuhusu mipango ya mafao ya wastaafu na kutekeleza sera zote za Serikali zinazohusiana na hilo.

Mamlaka inataka kuajiri wafanyakazi wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi:

| No. | Nafasi | Daraja | Idadi ya nafasi | Namba ya kazi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mkurugenzi, Ukaguzi wa Ndani na Uhakikisho ***Imetangazwa tena*** | RBA 2 | 1 | DIARA/01/01/2023 |
| 2. | Mkurugenzi, Usimamizi | RBA 2 | 1 | DS/02/01/2023 |

Maelezo ya nafasi hizo yanaweza kupatikana katika tovuti ya Mamlaka **www.rba.go.ke** na tovuti ya **https://recruitment.rba.go.ke/**

**Masharti ya Ofa:**
Mshahara mzuri unaolingana na majukumu ya nafasi hiyo utajadiliwa na wagombea waliofaulu.
Wagombea waliofaulu watateuliwa kwa mkataba wa miaka mitano (5) unaoweza kurejeshwa mara moja kwa kuzingatia utendakazi wa kuridhisha.

**Utaratibu wa Kutuma Maombi:**
Watu wanaovutiwa na wenye sifa stahiki wanapaswa kuwasilisha maombi yao kwa kuambatanisha na Wasifukazi wa kina (CV), nakala za vyeti/ushuhuda husika wa kitaaluma na nakala ya Kitambulisho cha Taifa. CV lazima angalau itoe maelezo ya barua pepe ya waombaji, nambari za simu za rununu za mchana, maelezo ya mwajiri wa sasa, malipo ya sasa na majina na mawasiliano ya waamuzi watatu (3).

Barua/maombi ya mtandaoni yanapaswa kutumwa kupitia tovuti ya e-recruitment **https://recruitment.rba.go.ke/** ya Mamlaka ambapo maombi ya kawaida yanapaswa kuwasilishwa katika ofisi za Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu zilizopo Rahimtulla Tower, Upper hill road, orofa ya 14 (Mapokezi) au kwa posta kupitia anwani ya posta iliyotolewa hapa chini. Maombi lazima yawe yamefungwa vizuri, yawekwe alama ya siri na marejeleo ya kazi husika yawekwe.

Maombi yote yanapaswa kushughulikiwa kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu**
**Rahimtulla Tower**
**P.O. Box 57733 - 00200 NAIROBI**

Lazima maombi yapokewe kabla ya Jumanne tarehe 14 Februari 2023

**Mahitaji ya Kuzingatia**:
Kwa mujibu wa Sheria ya (Marekebisho) ya Ajira, 2022, Mamlaka itawataka wagombea inaowataka kuingia nao mkataba wa maandishi kuzingatia sura ya sita ya Katiba kwa kuwasilisha vyeti vya lazima vya kufuata sheria na kibali kutoka kwa vyombo husika.

**Kwa mengi, tufuate katika:-**

**twitter: @RBA_Kenya**
**Instagram: rbakenya**
**facebook: @RetirementBenefitsAuthorityKE**
**linkedin: Retirement Benefits Authority Kenya**
**YouTube: Retirement Benefits Authority**
**Email: info@rba.go.ke**
**Website: www.rba.go.ke**

***Retirement Benefits Authority (RBA) is ISO 9001: 2015 Certified***

Funika mdomo unapopiga chafya
20 SEC Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza
Jitenge na walio na virusi
Usiguse macho, pua au mdomo na mikono michafu
Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi
Hakikisha maeneo yote ni safi
KOMESHA COVID-19



REPUBLIC OF KENYA

## KENYA MARINE AND FISHERIES RESEARCH INSTITUTE

## NAFASI YA KAZI

Kenya Marine and Fisheries Research Institute (KMFRI), ni Shirika la Kiserikali chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ushirika, Idara ya Uvuvi, Uzalishaji Samaki na Uchumi Bahar ini ilibuniwa na Sheria ya Bunge (The Science and Technology Act Cap. 250 of the Laws of Kenya of 1979) ambayo tayari imebatilishwa na The Science, Technology and Innovation Act No.28 of 2013.

KMFRI inataka kuajiri wataalamu wanaojituma ambao wanaweza kushirikiana na wenzao kujaza nafasi ifuatayo:

| S. No | Kazi | Idadi ya vyei | Gredi ya Kazi | Idara/Kitengo | Job Ref. No. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Katibu wa Shirika na Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria | 1 | KMFRI Grade 2 | Huduma za Kisheria | KMF/1 |
| | **Total** | **1** | | | |

**UTARATIBU WA MAOMBI**

Maelezo kamili ya tangazo na fomu ya maombi ya KMFRI zinapatikana katika sehemu ya 'Vacancies' kwenye tovuti ya KMFRI- **https://www.kmfri.go.ke**. Fomu ya kutuma maombi ya kazi inapasa kuwasilishwa kabla ya **Jumanne Februari 14, 2023.**

**b) MAHITAJI YA MAOMBI**

**Watakaofuzu watahitajika kutimiza matakwa ya Sura ya 6 ya Katiba kwa kutoka vyeti vifuatavyo:**

1. **Cheti cha Tabia Njema kutoka kwa Directorate of Criminal Investigations (DCI)**
2. **Cheti kutoka kwa Higher Education Loans Board (HELB)**
3. **Cheti cha kulipa ushuru kutoka Kenya Revenue Authority**
4. **Cheti kutoka Ethics and Anti-Corruption Commission (EACC)**
5. **Cheti kutoka Credit Reference Bureau (CRB)**

**c) UKUMBUSHO:**

1. Ni **WALE WANAOHITIMU** pekee tutawasiliana nao na watahitajika kutoka Kitambusho chao, vyeti vya masomo na vyeti vya taaluma wakati wa mahojiano.

2. Jaribio lolote la kujipigia debe litafanya ombi lako **LITUPWE MARA MOJA.**

***KMFRI NI MWAJIRI ANAYEZINGATIA USAWA MAKUNDI TOFAUT NA WATU WANAOISHI NA ULEMAVU, WANAWAKE, VIJANA NA WALE WALIOBAGULIWA WANAHIMIZWA KUTUMA MAOMBI.***

---

REPUBLIC OF KENYA

NAIROBI METROPOLITAN AREA TRANSPORT AUTHORITY
NaMATA Advancing Mobility

## TANGAZO LA ZABUNI

## IDHINI YA AWALI/ USAJILI KWA WASAMBAZAJI, WATOA HUDUMA NA WANAKANDARASI KWA USAMBAZAJI NA UTOAJI BIDHAA, HUDUMA NA KAZI KWA MUDA UNAOISHIA TAREHE 30 OKTOBA, 2024 NAMBA YA ZABUNI: NAMATA/PRQ/002/2022-2024

Mamlaka ya Usafiri wa Eneo la Jiji la Nairobi (NaMATA) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa kupitia Agizo la Mamlaka ya Usafiri wa Eneo la Metropolitan la Nairobi, 2017 (No.18 ya Kisheria ya tarehe 17 Februari 2017) likiwa na mamlaka ya kupanga, kudhibiti, na kuratibu usambazaji wa vifaa vya kutosha na Mfumo madhubuti wa Usafiri wa Umma wa Haraka kwa kusimamia uanzishaji wa Mfumo jumuishi, bora, bora na endelevu wa Usafiri wa Umma ndani ya Eneo la Jiji la Nairobi (NMA).

Kwa hivyo, Mamlaka inawaalika wagombeaji wanaostahiki na wanaovutiwa kutuma maombi ya kufuzu kabla na usajili wa Wasambazaji, Watoa Huduma na Wakandarasi kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Oktoba, 2024.

| NO. | NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | KUFUNGA/KUFUNGUA |
|---|---|---|---|
| 1. | NaMATA/PRQ/002/2022-2024 | Idhini ya awali/ Usajili kwa Wasambazaji, Watoa Huduma na Wakandarasi kwa Usambazaji na Utoaji wa Bidhaa, Huduma na Kazi kwa muda unaoishia tarehe 30 Oktoba, 2024. | Februari 21, 2023 |

Waombaji wanaostahiki wanaweza kupata maelezo zaidi na hati za usajili bila malipo kutoka kwa tovuti: www.namata.go.ke / www.treasury.go.ke au kununuliwa kutoka Idara ya Usimamizi wa Usambazaji, NaMATA baada ya kulipa isiyoweza kurejeshwa ya Shilingi Elfu Moja (Ksh.1,000.00), kwa kila seti ya hati zinazolipwa kwa Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Usafiri ya Eneo la Jiji la Nairobi. Waombaji wanaopakua Hati ya Kuhitimu sharti wapeleke maelezo yao mara moja kwa supplychain@namata.go.ke ili kuwezesha ufafanuzi au nyongeza yoyote zaidi.

Wazabuni wote wanaovutiwa wanatakiwa kuangalia mara kwa mara tovuti ya Mamlaka ya Usafiri ya Eneo la Jiji la Nairobi: www.namata.go.ke kwa nyongeza yoyote ya zabuni au ufafanuzi ambao unaweza kutokea kabla ya tarehe ya kuwasilisha.

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Usafiri ya Eneo la Jiji la Nairobi**

KENYA VISION 2030

---

REPUBLIC OF KENYA

## BODI YA MITIHANI YA TAASISI YA USAMBAZAJI (KISEB)

**KISM Towers, 11th Floor, Ngong Road,**
**P. O. Box 22873-00505, Nairobi, Kenya**
**info@kiseb.or.ke, www.kiseb.or.ke**
**Rununu: 0726 244828, 0769 878228**

KISEB Elevating Supply Chain

Bodi ya Mitihani ya Taasisi ya Usambazaji Kenya (KISEB) ni shirika lililoanzishwa na Sheria ya Usimamizi wa Wahudumu wa Usambazaji (SPM) ya 2007. Baraza la Mitihani limepewa jukumu la: kuagiza na kudhibiti silabasi za uthibitisho wa vifaa vya kitaaluma kwa watu wanaoomba usajili chini ya Sheria ya SPM; kuandaa na kusimamia mitihani kwa watu wanaotaka usajili chini ya Sheria ya SPM; kutoa vyeti vya kuhitimu kitaaluma na tuzo nyinginezo kwa watahiniwa ambao wamekidhi mahitaji ya mitihani.

## KATIBU/AFISA MKUU MTENDAJI; REF NO. KISEB 1/2023

Bodi ya KISEB ingetaka kuajiri kiongozi mwenye maono, mahiri na mbunifu aliye na kiwango cha juu viwango vya taaluma na maadili ili kujaza nafasi ya Katibu/Afisa Mtendaji Mkuu.

Kuripoti kwa Bodi ya KISEB, mgombea aliyefaulu atawajibika kutoa uongozi wa kimkakati, kuendesha ukuaji wa biashara katika uadilifu wa hali ya juu na mazingira ya kimaadili, kukuza sifa ya shirika na mwonekano na kuhakikisha ufanisi wa uendeshaji wa ufanisi.

**Majukumu/Kazi Muhimu**

i. Kutoa uongozi wa kimkakati kwa wafanyikazi wa KISEB;
ii. Kuongoza uundaji na utekelezaji wa sera na taratibu zinazofaa zinazoipa KISEB mtazamo na chanya na faida ya ushindani;
iii. Kuwajibika kwa shughuli za kila siku za KISEB;
iv. Kusimamia timu za ndani za fani mbalimbali ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafiwa;
v. Kuwezesha utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya kimkakati na ya mwaka ya KISEB;
vi. Kuwezesha kuripoti mara kwa mara juu ya hali ya utendaji wa KISEB;
vii. Kuwajibika kwa utekelezaji na mawasiliano ya mikakati, maamuzi na sera za Bodi;
viii. Kuhakikisha kuwa shirika lina muundo bora wa usimamizi ikijumuisha mipango ya urithi;
ix. Kuratibu uhamasishaji wa rasilimali ili kuongeza utimilifu wa malengo ya kimkakati;
x. Kukuza uhusiano na wizara husika, washirika wa maendeleo na wadau wengine kwa manufaa ya KISEB;
Xi. Kuhakikisha usimamizi wa busara wa rasilimali zote zilizopo za KISEB;
xii. Kuhakikisha uzingatiaji wa mikataba na mikataba husika ya kitaifa na kimataifa;
xiii. Kukuza utamaduni mzuri wa ushirika unaokuza maadili na utawala bora kulingana na Katiba ya Kenya 2010;
xiv. Kuratibu utayarishaji wa taarifa za bajeti na fedha kwa ajili ya kuzingatiwa na kuidhinishwa na Bodi;
xv. Kukuza mitandao na ushirikiano na washirika wa maendeleo na ushirikiano wa wafadhili wakuu, uchangishaji fedha na maendeleo ya mradi ndani ya KISEB;
xvi. Kuhakikisha uzingatiaji wa sera na miongozo ya udhibiti na maagizo ya Serikali.
xvii. Kuwa kiungo kati ya Bodi na Menejimenti na wadau wengine;
xviii. Kuwajibika kwa usimamizi wa washikadau na uboreshaji wa taswira ya shirika ya shirika.

**Umahiri wa Kazi (Maarifa, Uzoefu na Sifa/Ujuzi)**

i. Lazima uwe na shahada ya digrii katika elimu, ununuzi, ununuzi na vifaa,fedha, biashara, usimamizi au shahada yoyote inayohusiana na chuo kikuu kinachotambulika.

ii. Lazima uwe na digrii ya bwana katika usimamizi wa ununuzi au ugavi.

iii. Lazima uwe mwanachama aliyesajiliwa wa shirika la kitaaluma na mwenye leseni halali ya mazoezi.

iv. Awe na uzoefu wa angalau miaka kumi na tano (15) ambapo miaka mitano lazima awe katika nafasi ya usimamizi mkuu, ikiwezekana katika sekta ya umma.

v. Awe na ujuzi na uzoefu katika utungaji wa sera, usimamizi na taratibu zinazowezekana kutoka kwa sekta ya umma;

vi. Awe amefanya kozi ya uongozi kutoka katika taasisi inayotambulika;

vii. Ustadi katika teknolojia ya mawasiliano ya habari.

viii. Anapaswa kuwa na ustadi bora wa mawasiliano na uwasilishaji, uwezo dhabiti wa kibinafsi, uchambuzi, shirika na timu na hadhi ya juu ya maadili ya kitaaluma.

ix. Lazima ikidhi matakwa ya Sura ya Sita ya Katiba kuhusu uadilifu na uongozi.

**Masharti ya Uajiri**: Uteuzi ni wa masharti ya huduma ya kimkataba yenye ushindani.

**Jinsi ya Kutuma Maombi**: Waombaji wanapaswa kutuma CV zao za kina, nakala za vyeti husika na ushuhuda, anwani ya barua pepe, nambari za simu za mchana na majina ya wadhamini watatu (3) ili kufikia waliosainiwa chini kabla au **Jumanne tarehe 7 Februari 2023.**

**Mwenyekiti,**
**Bodi ya Mitihani ya Taasisi ya Usambazaji Kenya (KISEB)**
**KISM TOWERS, Orofa ya 11, Barabara ya Ngong**
**P. O. Box 22873-00505,**
**Nairobi, Kenya,**
**ceorecruitment@kiseb.or.ke**

KENYA VISION 2030

“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”




EXPRESSION OF INTEREST (EOI)

REPUBLIC OF KENYA

KenGen
Kenya Electricity Generating Company PLC

# MWALIKO WA ZABUNI (EOI) KWA HUDUMA ZA USHAURI KWA KUFANYA UTAFITI WA UWEZEKANO WA UPANDAJI WA KUKAVU WA HEWA YA HYBRID WA MASHAMBA MAKUBWA YA OLKARIA GEOTHERMAL

## (Wazi Kimataifa)

**1. Usuli.**

Kampuni ya Kuzalisha Umeme ya Umma Kenya (KenGen) iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni,. Serikali ya Jamhuri ya Kenya ilimiliki asilimia 70%. Umma unamiliki hisa 30% kama ilivyoorodheshwa kwenye The Soko la Hisa la Nairobi. KenGen iliyojumuishwa mwaka wa 1954 ilipewa jukumu la kuendeleza, usimamizi na uendeshaji wa mitambo ya nishati ya jotoardhi.

Chini ya udhibiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mafuta ya Nishati (EPRA) KenGen iliingia katika Mkataba wa Ununuzi wa Umeme mahususi na Kampuni ya Umem Kenya (KPLC). KenGen ilipata leseni ya wizara ya nishati kwa unyonyaji wa rasilimali ya jotoardhi yenye urefu wa kilomita 204 huko Naivasha. KenGen ilizalisha takriban 75% ya umeme unaotumika nchini, huku mchango wa vyanzo vya jotoardhi wa takriban 48% ya GWh 8442.97 zilizouzwa katika mwaka wa fedha wa 2021 kutokana na rasilimali ya jotoardhi iliyoko Olkaria, NAIVASHA na Eburru, Gilgil na kila moja ya uwezo wa 796.7 MW. na MW 2.3 mtawalia. Vyanzo vingine vya kuzalisha umeme ni kati ya mitambo ya maji, mitambo ya nishati ya joto na vinu vya upepo. KenGen PLC jumla ya uwezo uliosakinishwa wa MW 1,818 kando na mauzo ya 96% ya umeme kutoka kwa vyanzo vya nishati mbadala: jotoardhi, upepo na maji. Mkakati wa upanuzi wa uzalishaji wa umeme wa KenGen unazingatia teknolojia safi. huku ikiboresha matumizi ya rasilimali zilizopo.

Chini ya Dira ya 2030, Serikali ya Kenya inatarajia kuongeza uwezo wa umeme uliowekwa kutoka MW 2,298 hadi MW 17,764 kufikia mwaka wa 2030 ili kukidhi makadirio ya mahitaji ya nishati ya 8% kwa mwaka. Uzalishaji kutoka kwa rasilimali ya jotoardhi unatarajiwa kuchukua jukumu kuu katika mpango huu ili kushughulikia kuongezeka kwa usawa wa mahitaji ya usambazaji wa nishati huku kupunguza utoaji wa kaboni unaohusishwa na uzalishaji wa kawaida wa umeme.

Kufuatia hili, KenGen, pamoja na Serikali, inapanga kuongeza uwezo wa nishati ya jotoardhi hadi MW 1260 ifikapo mwaka wa 2022. KenGen inakusudia kushirikisha huduma za ushauri za kampuni iliyohitimu na yenye uzoefu kwa kufanya upembuzi yakinifu wa upozeshaji mseto wa hewa ukavu unaolenga maeneo makubwa zaidi ya jotoardhi ya Olkaria ili kuhakikisha utumizi wa gharama nafuu, ubora na endelevu wa kimazingira wa rasilimali zilizothibitishwa za jotoardhi.

**2. Malengo.**

Ili kufikia lengo hili, kampuni inalenga kushirikisha huduma za ushauri za makampuni yanayotambulika ili kufanya upembuzi yakinifu wa kina kuhusu upoaji mseto wa hewa kavu kwa kujumuisha data ya matumizi ambayo imekuwa ikipatikana tangu utafiti uliopita.

Kwa ujumla, malengo ya utafiti ni:

1) Kukagua matokeo yanayopatikana ya kemia, utendakazi wa mifumo ya kukusanya stima, na mitambo ya kuzalisha umeme kando na data iliyopo (ripoti za awali za utafiti, tathmini za awali za rasili mali na mazingira, hali ya utendakazi na seti za data za matumizi ya rasilimali, na data na ripoti nyingine zozote zinazofaa). Usha juu ya mapungufu ya ziada ya data yanayohitajika ili kufanya utafiti wa uboreshaji kwa mafanikio. Mshauri wa kuonyesha mbinu zao kwa kuwa hakuna mbinu inayopendekezwa inatolewa.
2) Kutambua teknolojia inayofaa, na eneo kwa ajili ya kubuni, ujenzi na uendeshaji wa mnara wa mseto wa kupozea hewa kavu na condenser kwa kuzingatia mahitaji ya alama za miguu (ukubwa, na mpangilio wa mimea) na uwiano wa uhifadhi wa maji. Shauri juu ya mpangilio mzuri zaidi wa mradi na usanidi.
3) Kufanya uigaji wa nambari wa minara ya mseto ya kupoeza hewa kavu ili kutabiri utendakazi wa kikondoo, uzalishaji wa nishati, mahitaji ya upakiaji kisaidizi kulingana na hali ya mazingira ya sasa na ya baadaye.
4) Kushauri juu ya maendeleo bora zaidi ya minara ya kupoeza kwa ajili ya mitambo mahususi ya umeme iliyokabidhiwa kwa ajili ya kuiga ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya mpango endelevu wa matumizi ya rasilimali kuhusiana na
   (i) Ufanisi bora zaidi wa mvuke kwa kila mzunguko wa Mchakato wa megawati
   (ii) Pato bora (MW) kulingana na uigaji wa saizi ya mmea,
   (iii) Mkakati wa urejeshaji sindano kwa uwanja mzima
5) Ili kutekeleza makadirio ya gharama basi tengeneza muundo wa dhana wa mnara wa kupoeza na unaohusishwa miundombinu ikiwa ni pamoja na kuweka upya mitambo iliyopo kwa kila megawati inayozalishwa katika kila moja jenereta.
6) Kuzingatia gharama za mtaji na matumizi ya uendeshaji
7) Kufanya uchambuzi wa kiuchumi na kifedha kwa ajili ya uchaguzi wa teknolojia ili kutekeleza upoaji mseto wa hewa kavu mnara, na kutathmini adhabu za utendakazi zinazoweza kupatikana kama ilivyoainishwa katika dhima ya makubaliano ya ununuzi wa Nishati kutokana na makadirio ya asilimia ya kushuka kwa uzalishaji wa nishati.
8) Kufanya Ripoti ya Utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya minara iliyopendekezwa ya kupozea hewa mseto.
9) Kushiriki katika angalau mkutano mmoja wa kimwili utakaofanyika nchini Kenya na mikutano miwili ya mtandaoni kwa wakati uliopangwa kuhusu vipengele vinavyohusika vya shughuli za maendeleo ya jotoardhi, michakato na mazoea yanayohusiana na mgawo huo.
10) Kufanya uhamishaji wa teknolojia na kuwajengea uwezo wafanyakazi wenza wa mteja waliopewa mradi mseto wa kupozea hewa kavu unaozingatia matengenezo ya mifumo ya ndani na uwezo. Idara ya Uendeshaji itakuwa mtumiaji wa mwisho. Idadi inayokadiriwa ya watumiaji ni hamsini (50) chini ya uthibitisho kulingana na asili ya zana na mipango inayopendekezwa.

**3. Wigo wa Huduma**

Ili kufikia lengo hili, kampuni inataka kushirikisha huduma za makampuni ya ushauri yenye sifa nzuri ili kutekeleza utafiti wa kina wa uboreshaji na uundaji wa nambari za hifadhi ili kufikia eneo la jotoardhi la Kilomita 204 Kubwa la Olkaria, utafiti utajumuisha data mpya ya uchunguzi na matumizi ambayo imekuwa ikipatikana tangu utafiti wa mwisho katika eneo la jotoardhi Kubwa la Olkaria na mawanda yaliyoelezwa hapa chini.

1. Kagua data iliyopo kuhusu kemia (tathmini za zamani za rasilimali na mazingira na ripoti); mifumo ya kukusanya stima, na hali ya mitambo ya uendeshaji na seti za data za matumizi ya rasilimali, na data na ripoti zingine zozote muhimu)
2. Ushauri juu ya data na tafiti za ziada zinazohitajika ili kufanya utafiti wa uboreshaji kwa mafanikio. Mshauri waonyeshe mbinu zao kwani hakuna mbinu inayopendekezwa.
3. Uamuzi wa uwezo bora zaidi, utambulisho wa chaguo zinazofaa za teknolojia, mahitaji ya alama za miguu (ukubwa, eneo, na mpangilio bora wa mimea) na uwiano wa uhifadhi wa maji kama mchakato wa ubunifu katika kubuni, ujenzi na uendeshaji wa minara ya mseto ya kupozea hewa kavu. .
4. Tekeleza uigaji wa nambari wa minara ya mseto ya kupoeza hewa kavu ili kutabiri utendakazi wa kiboreshaji, uzalishaji wa umeme, mahitaji ya mzigo msaidizi katika kukabiliana na hali ya mazingira ya sasa na ya baadaye.
5. Tengeneza muundo dhahania wa minara ya mseto ya kupozea hewa kavu na miundombinu inayohusiana.
6. Kufanya uchambuzi wa kiuchumi na kifedha wa chaguzi za maendeleo zilizopendekezwa. Adhabu za utendakazi ambazo zinaweza kupatikana kama ilivyoainishwa katika dhima ya makubaliano ya ununuzi wa Nishati kwa sababu ya uzembe wa mfumo kutokana na makadirio ya kushuka kwa asilimia katika uzalishaji wa nishati.
7. Gharama ya mtaji na matumizi ya uendeshaji kuzingatiwa kwa uchaguzi wa teknolojia ya kutekeleza upoaji hewa kavu katika mimea ya jotoardhi ya Olkaria; Ufanisi wa gharama ya kuweka upya mitambo iliyopo kwa kila megawati inayozalishwa katika kila jenereta. Tathmini utendaji wa mfumo wa uchimbaji wa gesi.
8. Ripoti ya Utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya minara iliyopendekezwa ya mseto ya kupozea hewa kavu.
9. Shiriki katika angalau mikutano ya kimwili itakayofanyika nchini Kenya na mikutano miwili ya mtandaoni kwa nyakati zilizopangwa kuhusu vipengele vinavyohusika vya shughuli za maendeleo ya jotoardhi, michakato na mazoea yanayohusiana na mgawo huo.
10. Tekeleza uhamishaji wa teknolojia na kuwajengea uwezo wafanyakazi wenza wa mteja waliopewa mradi mseto wa kupozea hewa kavu unaozingatia matengenezo ya mifumo ya ndani na uwezo. Idara ya Uendeshaji itakuwa mtumiaji wa mwisho. Idadi inayokadiriwa ya watumiaji ni hamsini (50) chini ya uthibitisho kulingana na asili ya zana na mipango inayopendekezwa.

**4. Nyaraka Zinazohitajika**

a) Toa mahitaji yaliyo hapa chini;
   - Jina la kampuni
   - Anwani ya makazi
   - Barua pepe
   - Kuwasiliana na mtu
   - Anwani ya posta
   - Nambari ya simu

b) Nakala zilizoidhinishwa za vyeti/nyaraka za usajili wa kampuni ili kuthibitisha hali ya kisheria katika nchi ya makazi; aidha, pale ambapo mzabuni ni muungano, mkataba wa muungano uliotiwa saini ambao lazima ubainishe wajibu wa kila upande katika muungano. (Si zaidi ya makubaliano ya muungano wa kampuni moja kwa EOI hii yataruhusiwa).
c) Cheti cha usajili (na cheti chochote cha mabadiliko ya jina), kuthibitishwa na mwakilishi aliyeidhinishwa wa mzabuni au (kama itakavyokuwa) mwanachama wa muungano.
d) Nakala zilizoidhinishwa za Memorandum/Articles of Association kwa wanachama wote wa muungano.
e) Pale ambapo Mwombaji ni muungano, orodha ya wanachama wanaopendekezwa wa muungano na Kiongozi anayependekezwa wa muungano. (Ambatanisha makubaliano ya muungano).
f) Wanachama wote wa muungano lazima watimize mahitaji ya EOI
g) Taarifa kuhusu shauri lolote la sasa linalohusisha kampuni ya ushauri iliyoidhinishwa na kampuni inayotambulika ya sheria.

**5. Vigezo vya Kustahiki**

Kando na wahusika wanaovutiwa (kampuni, wataalamu, au muungano) kutokuwa na nia ya kandarasi zinazotolewa na KenGen, au katika mashirika yanayofanya kazi au kupendekeza kufanya kazi kwa KenGen. Wahusika (makampuni, wataalam, au muungano) wanapaswa kutii Sheria ya Ununuzi wa Umma na Usambazaji wa Mali ya 2015 Sehemu ya X, masharti ya Kifungu cha 130 kuhusu maslahi yanayokinzana. Zaidi ya hayo, makampuni, wataalam au vyama vinavyovutiwa vitakidhi vigezo vilivyoorodheshwa hapa chini:

a) Mzabuni lazima atoe ripoti mbili (2) za hivi punde zilizokaguliwa za kila mwaka na kampuni ya ushauri inayoheshimika.
b) Maelezo ya muundo wa usimamizi/shirika, orodha ya wafanyakazi wakuu wanaohusika na kazi a walio na sifa za chini zaidi za kitaaluma za shahada ya sayansi (mazingira; jiokemia), uhan(uraia, mitambo, umeme, nguvu), uchumi, au sawa;
c) Uzoefu wa kibinafsi wa wafanyikazi wakuu wa angalau miaka kumi katika rasilimali ya jotoardhi modeli, tathmini, usimamizi na uendeshaji wa nguvu, tathmini ya mazingira. Wasifu wao (CV) ikijumuisha uzoefu wa kitaaluma na kitaaluma lazima uambatishwe kwenye hati ya zabuni. Sifa za jumla, uidhinishaji na Ushahidi wa uzoefu wa mtu binafsi katika nyanja zinazohusiana na jotoardhi (angalau miaka 20) Nakala za vyeti vilivyowasilishwa zinapaswa kuthibitishwa kulingana na matakwa ya nchi ya mtaalam. Kwa mfano, Vyeti vya wataalamu wa Kenya vinaweza kuthibitishwa na kamishna wa viapo.
d) Ufichuaji wa madai ya sasa (ikiwa yapo) yanayohusisha pande zinazoshauriana (kampuni, wataalamu, au muungano) iliyoidhinishwa na kampuni ya mawakili inayotambulika.
e) Wahusika wanaovutiwa (makampuni, wataalam, au muungano) wanapaswa kuwa na uzoefu wa miaka Mitano (5). uundaji wa rasilimali za jotoardhi, tathmini, upangaji na uendelezaji wa mradi wa umeme, tathmini ya mazingira. Toa barua za marejeleo zinazoelezea kazi mahususi. Ambatanisha angalau tatu barua za pongezi kutoka kwa watengenezaji wa huduma za umeme na/au waendeshaji kwa kutekeleza sawa huduma. Ushahidi wa marejeleo makuu matatu ya wateja.
f) Utiifu halali wa kodi au hati sawa ya kisheria kwa wazabuni wa kimataifa.
g) Ushahidi wa usajili kama makampuni, mtaalam, au muungano. Wahandisi, wanasayansi na wataalamu wengine wanapaswa kusajiliwa na chombo cha kitaaluma kama inavyotakiwa na mamlaka husika.
h) Ushahidi wa uhamishaji wa uwezo wa maarifa

**6. Ufafanuzi**

Watu wanaovutiwa wanaweza kuomba ufafanuzi juu ya mchakato huu wa Uonyeshaji wa Maslahi kwa hadi siku Saba (7) kabla ya tarehe ya kuwasilisha. Ombi lolote la ufafanuzi lazima litumwe kwa maandishi kwa karatasi, barua, au barua ya kielektroniki kwa:

**Meneja Mkuu, Mfumo wa Usambazaji,**
**Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya PLC,**
**Orofa ya 9, Stima Plaza, Phase 2, Barabara ya Kolobot, Parklands,**
**P.O. BOX 47936-00100 GPO Nairobi, Kenya**
**Simu: 254-020-3666204**
**Barua pepe: tenders@kengen.co.ke; CC: Ponyango1@kengen.co.ke; pmangi@kengen.co.ke.**

**7. Uwasilishaji**

Nakala tatu (3) za hati za kufuzu zitawasilishwa zikiwa na alama ya wazi **HALISI (1)** na **NAKALA (2)** katika bahasha tofauti zilizofungwa. Kila bahasha inapaswa kuandikwa kwa uwazi ***“KGN-GDD-05-2023-SIRI - MWALIKO WA ZABUNI (EOI) KWA HUDUMA ZA USHAURI KWA KUFANYA UTAFITI WA UWEZEKANO WA KUPOOZA KUKAVU HEWA HYBRID WA UWANJA MKUBWA WA OLKALIA GEOTHERMAL”***

Hati za kuhitimu lazima ziwasilishwe kwa mkono au barua iliyosajiliwa kwa:

**Meneja Mkuu, Mfumo wa Usambazaji,**
**Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya PLC,**
**Orofa ya 9, KenGen Pension Plaza II,**
**Barabara ya Kolobot, Parklands,**
**P.O. Box 47936, 00100**
**NAIROBI**

Hati za EOI zinapaswa kuwekwa kwenye sanduku la zabuni lililo kwenye Orofa ya Chini ya KenGen, jengo la RBS. Zabuni ambazo haziwezi kutoshea kwenye kisanduku cha zabuni zinapaswa kuwasilishwa kwa Meneja Mkuu - Ofisi ya Mfumo wa Usambazaji iliyoko kwenye Orofa ya 9 ya KenGen Plaza II kabla au tarehe ya mwisho ya kuwasilisha.

Wazabuni wanapaswa kuwasilisha nakala moja halisi na Nakala (2) ya EOI mnamo au kabla ya tarehe 14 Februari 2023 saa 10.00 asubuhi. EOI itafunguliwa siku hiyo hiyo hadharani saa 1030, (saa za Kenya) katika Orofa ya 6, KenGen Pension Plaza. II mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaoamua kuhudhuria.

Hati ya Zabuni pia inaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti yetu **www.kengen.co.ke**
Wazabuni wanashauriwa kuwa wakiangalia tovuti mara kwa mara hadi siku saba (7) kabla ya tarehe ya kuwasilisha taarifa zozote zilizopakiwa kupitia ufafanuzi/nyongeza.
Kampuni zilizohitimu mapema chini ya utaratibu huu pekee ndizo zitakazoalikwa kuwasilisha mapendekezo yao ya Kiufundi na Kifedha chini ya Ombi la Mapendekezo (RFP).

KenGen inahifadhi haki ya kukubali au kukataa maombi yoyote au yote bila wajibu wa kutoa sababu yoyote ya uamuzi. Watu waliohitimu awali chini ya utaratibu huu pekee ndio watakaopewa hati za zabuni na wataalikwa kuwasilisha zabuni zao za kiufundi na kifedha chini ya Ombi la Mapendekezo (RFP).

**MENEJA MKUU, MFUMO WA UGAVI**






# KENHA yazidisha msako wa madereva wa kubeba miwa wanaosababisha ajali

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu Kenya (KeNHA) imeanza msako wa wa madereva watundu wa miwa ili kuzuia uharibifu wa barabara katika eneo la Nyanza.

Hii inafuatia ongezeko la idadi ya visa, miongoni zikiwa ajali, zinazohusisha malori ya miwa na malori na kusababisha uharibifu wa barabara muhimu za Mamlaka hiyo.

Meneja wa KeNHA eneo la Nyanza, Mhandisi Julius Mak'oderoh, alilaumu ajali hizo kwa uhuru ambao madereva hao wamepatiwa na kampuni za kusaga miwa, na kuifanya vigumu kwao kufuatilia na kubaini shughuli zao barabarani wakisafirisha miwa.

"Kampuni za sukari zimetafuta huduma hizi nje kwa kupatia kandarasi kampuni za usafirishaji. Tunapowaendea kuhusu masuala haya, wanadai hawawezi kuwa na uthibiti," alisema.

Madereva hao, alisema, wana tabia ya kupuuza sheria za barabarani hasa wanapokaribia daraja ili waweze kupata nguvu za kupanda mlima na kusababisha ajali.


Tinga tinga inayobeba miwa

Hasa alitaja daraja la Kasagam, ambapo malori kadha ya miwa yameanguka kwa sababu ya tabia ya madereva.

